SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.21 NO. 1 2022
DOI: 10.51984/JOHS.v21I1.1602

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs

# Taswira Na Vikwazo Kwa Wanawake Katika Riwaya Teule Za Ben Mtobwa.

Saad Buoazuom Mehemed

African Languages, Faculty of Arts, Sebha University, Libya

**Keywords:**
Wanawake
Mazingira
Riwaya
Tabia
Mbalimbali
Makala
Malengu

**ABSTRACT**

Makala haya yamelenga kuangalia vikwazo anavyokumbana navyo mwanamke katika kupata maendeleo kama vilivyosawiriwa na Ben R. Mtobwa. Maswala yanayosawiriwa katika riwaya teule za Ben Mtobwa ni taswira halisi ya mambo yanayoendelea katika jamii zetu za leo. Riwaya zilizochambuliwa katika Makala haya ni Salamu Kutoka Kuzimu (1984), Tutarudi na Roho Zetu (1987), Dar es Salaam Usiku (1998) na Mtambo wa Mauti (2004). Makala haya yanalenga kuchambua vikwazo vinavyowarudisha wanawake nyuma katika harakati zao za kupigania usawa. Ben R. Mtobwa katika kusawiri wanawake anaweka wazi changamoto wanazokutana nazo wanawake katika kufikia ndoto zao na kwamba mazingira ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na hata kiutamaduni yanachangia kwa kiasi kikubwa kuwarudisha nyuma. Nadharia iliyotumika katika Makala hii ni Ufeministi wa Kiafrika. Nadharia hii hueleza matatizo na changamoto wanazopitia wanawake wa Kiafrika na namna ya kutatua changamoto hizo. Aidha taswira za wanawake katika riwaya hizi za Ben Mtobwa zinaonesha kwamba mwandishi anakinzana na misingi ya nadharia ya kifeministi mathalani Ufeministi wa Kiafrika katika kumchora mwanamke wa Kiafrika lakini anaweza akawa anawaamsha wanawake wa Kiafrika kwa namna moja au nyingine kwa kuweka wazi vikwazo na changamoto zinazowazuia katika kufikia malengo ya harakati za kifeministi. Mwisho kabisa, makala haya yanapendekeza nini kifanyike ili kuwanusuru wanawake na vikwazo hivyo vilivyochambuliwa katika riwaya teule.

# الصوروالعقبات أمام النساء في رواية بن متوبوا

سعد ابوعزوم امحمد علي

قسم اللغات والدراسات الإفريقية، كلية الأداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
المرأه
طبيعة
الادب
العادات
مختلفة
المقالة
الرواية
نضرية
الاهداف.

**الملخص**

تهدف هذه المقالة إلى إلقاء نظرة على العوائق التي تواجهها المرأة في تحقيق التنمية كما أوضحها بن متوبوا. إن القضايا التي تم تصويرها في روايات بن متوبوا المختارة هي انعكاس حقيقي لما يجري في مجتمعاتنا اليوم. الروايات التي تم تحليلها في هذا المقال هي تحية من الجحيم (1984) ، وسنعود بأرواحنا (1987) ، وليلة دار السلام (1998) ونبتة الموت (2004). تهدف هذه المقالة إلى تحليل العوائق التي تعوق النساء في سعيهن لتحقيق المساواة. يسلط بن متبوا في تصوير المرأة الضوء على التحديات التي تواجهها المرأة في تحقيق أحلامها وأن السياقات الاجتماعية والسياسية والاقتصادية وحتى الثقافية تساهم بشكل كبير في إعاقتها. النظرية المستخدمة في هذا المقال هي النساء الأفريقيات. تصف هذه النظرية المشاكل والتحديات التي تواجهها المرأة الأفريقية وكيفية حلها. بالإضافة إلى ذلك ، لكنه قد يوقظ النساء الأفريقيات بطريقة أو بأخرى من خلال كشف الحواجز والتحديات التي تمنعهن من ذلك تحقيق أهداف الحركة النسائية.

في نصوص مختلفة ، تم تصوير المرأة في مجموعة متنوعة من السياقات الإيجابية أو السلبية بناءً على تجاربها في الحياة والسلوكيات المختلفة أو رؤية المجتمع الذي تعيش فيه (Ndungo ، 1985؛ Chesaina ،

*Corresponding author:
E-mail addresses: saa.ali@sebhau.edu.ly

*Article History : Received 07 November 2021 - Received in revised form 28 February 2022 - Accepted 09 March 2022*

1987؛ Kimani، 2003؛ Gitau، 2005). هذه الصور في هذه النصوص هي واقع المرأة في مجتمع اليوم وأن تحول هذه الصور يسير جنبًا إلى جنب مع جهود النساء أنفسهن في الكفاح من أجل المساواة .
يُنظر إلى صور النساء في الأعمال الأدبية المختلفة على أنها صورة سلبية في المجتمع بسبب حقيقة أن معظم الأعمال الأدبية كتبها رجال وأنهم كتبوا وفقًا لتجاربهم الذكورية.

## UTANGULIZI

Katika maandiko mbalimbali, wanawake wamekuwa wakichorwa katika taswira mbalimbali zenye kupendeza au zisizopendeza kulingana na tajiriba zao katika maisha mbalimbali na mwenendo au dira ya jamii ambamo wanaishi (Ndungo, 1985; Chesaina, 1987; Kimani, 2003; Gitau, 2005). Taswira hizi katika maandiko hayo ndio uhalisia wa mwanamke katika jamii ya leo na kwamba kubadilika kwa taswira hizo kunaenda sawia na juhudi za wanawake wenyewe katika kupigania usawa.

Taswira za wanawake katika kazi mbalimbali za fasihi zimekuwa zikionekana kama taswira hasi katika jamii kutokana na ukweli kwamba kazi nyingi za fasihi zinaandikwa na wanaume na wanaandika kwa kulingana na tajiriba zao za kiume. Mjadala juu ya usawa baina ya wanawake na wanaume umekuwa muhimu sana katika zama hizi na baadhi ya waandishi wanatumia nafasi hii kumchora mwanamke katika taswira yenye heshma ndani ya jamii lengo kuu likiwa ni kupigania usawa wa kijinsia. Kuwachora au kuwasawiri wanawake kama wahusika wenye uwezo mkubwa na wanaofaa kuigwa katika jamii ni miongoni mwa jitihada zinazowekwa na wasanii au waandishi wenye itikadi za kifeministi ili kuielimisha jamii nzima juu ya usawa wa kijinsia.

Makala haya yanadhamiria kuchunguza riwaya teule za Ben Mtobwa ili kuona namna zinavyosawiri vikwazo vinavyowakabili wanawake katika kufikia ndoto zao. Makala haya yataangalia jinsi mwandishi anavyosawiri wahusika wa kike katika riwaya hizi kwa kuangalia vikwazo wanavyokumbana navyo katika harakati za kufikia ndoto zao. Benard Rashid Mtobwa ni mwandishi wa kazi za sanaa anaefahamika kimaandishi kama Ben Mtobwa. Alizaliwa katika kijiji cha Ujiji katika mkoa wa Kigoma mnamo Agosti mwaka 1958 (Gromov, 2008). Miongoni mwa kazi zake za sanaa ni riwaya ya *Nitakusubiri* (1992), *Zawadi ya Ushindi* (1997), *Dar es Salaam Usiku* (1998) na riwaya zingine nyingi. Katika kazi zake nyingi, Ben Mtobwa anawajenga wahusika wake katika mazingira yaliyojaa misukosuko ya maisha. Hivyo makala haya yatachunguza vikwazo vinavyowakumba wahusika wa kike katika riwaya teule za Ben Mtobwa na jinsi vikwazo hivyo vinavyowazuia kufikia ndoto zao. Nadharia iliyotumika kufanya uchambuzi katika makala haya ni nadharia ya Ufeministi wa Afrika.

**Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika**

Makala haya yanaongozwa na nadharia maalumu ya Ufeministi wa Kiafrika. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika huangazia zaidi katika matatizo na changamoto za maisha wanazokumbana nazo wanawake wa Kiafrika, chanzo cha matatizo hayo na njia za kuepukana nayo. Steady (1981) ambaye ndiyo mwasisi wa nadharia hii anaeleza kwamba miongoni mwa changamoto anazokumbana nazo mwanamke wa Kiafrika ni pamoja na kukosa uhuru juu ya masuala ya ndoa, ukeketaji wa wanawake (FGM), kukosa uhuru wa kujieleza au unyamavu wa kulazimishwa kama anavyouita Pamela, (2016), urithi wa mila na desturi, kunyimwa haki ya elimu pamoja na unyanyasaji wa wanawake tasa. Steady (1981) anaeleza kuwa Ufeministi unapohusishwa na fasihi ya Kiafrika unafaa kuchunguza hali za kijamii na kiutamaduni zinazochangia katika unyanyasaji wa wanawake wa Kiafrika. Makala haya, yamerejelea mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kama ilivyoorodheshwa na Steady (1981) na kunukuliwa na Pamela (2016).

a) Mwanamke wa Kiafrika ana uwezo wa kujitegemea na kuishi bila ya kudhulumiwa;

b) Mwanamke wa Kiafrika ana nafasi kubwa katika ujenzi wa jamii ambayo yeye ni mshiriki;

c) Mwanamke wa Kiafrika anaweza kuwa shujaa na hata mtawala;

d) Uhalisia wa wanawake wa Kiafrika unadhihirika katika fasihi ya Kiswahili.

Kwa ujumla, nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni miongoni mwa matawi ya nadharia pana ya Ufeministi ambayo imejikita na kuelekeza nguvu na nia katika kupigania ukombozi wa mwanamke katika jamii mbalimbali kutokana na pingu za kiuchumi, kijinsia, kidini, kisiasa, kijamii na kiutamaduni, (Wamitila, 2003). Katika kuchunguza chanzo cha matatizo yanayowakumba wanawake, anaeleza Wamitila, (2003), nadharia ya Ufeministi imekuwa ikijikita zaidi katika kuchunguza misimamo na itikadi za kiume ambazo zimekuwa kikwazo kibwa cha wanawake dhidi ya maendeleo katika jamii mbalimbali.

Njogu na Chimerah (1999) wakikariri mawazo ya Cheri Register katika kitabu cha Ruthven (1990), ambae ni miongoni mwa waasisi wa Ufeministi, wanadai kwamba nadharia hii:

a) Hutumia fasihi kuanika na kueleza kwa kina hali anazokumbana nazo mwanamke ili jamii nzima iweze kuelewa.

b) Hutangaza nia ya kuleta usawa wa kiutamaduni na kijinsia. Inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinadamu bila kujali maumbile;

c) Huhamasisha wasanii wa kazi za sanaa kutumia wahusika wa kike ambao ni mashuhuri, hawategemei wanaume, na ni mfano wa kuigwa katika jamii.

d) Huamini kwamba jinsia ndio msingi wa mahusiano ya kijamii na kwamba maisha hutegemea katika jinsia zote mbili, yaani ya kike na ya kiume.

e) Hufufua fasihi ya kike katika fasihi ya Kiswahili kwa kuweka wazi kazi za sanaa zilizotungwa na wanawake na ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanaume.

Katika kupigania usawa wa kijinsia, wanawake wa Kiafrika huwa na udhaifu fulani unaowakwamisha katika harakati zao. Mfano, Ogundipe-Leslie (1984) anaeleza kuwa matatizo yanapomkumba mwanamke wa Kiafrika huonyesha uoga, mielekeo ya kutaka kuwafurahisha wengine na kubembeleza badala ya kutenda vitendo vya kutetea haki. Katika kuchambua riwaya za Ben Mtobwa, makala haya yamegundua vikwazo vifuatavyo wanavyokumbana navyo wanawake.

## VIKWAZO VYA KIUCHUMI

Mwandishi amewasawiri baadhi ya wanawake warembo wakifanya ukahaba kama njia yao ya kujipatia kipato na kujikwamua kutoka kwenye hali ngumu ya kiuchumi. Mwandishi anawasawiri wanawake hao kama zao la mazingira ya kifukara kitu ambacho kimefanya wajiingize kwenye biashara ya ngono kwa matarajio ya kupata kipato kitakachoweza kuwaondoa katika wimbi la umasikini. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984), tunamuona *Waridi*, binti aliyelelewa katika mazingira magumu ikiwemo kwenye madanguro ambamo mama yake mzazi alikuwa akifanya biashara ya ngono. Kimsingi, mwandishi Ben Mtobwa anasawiri barabara namna mazingira yanavyowaweka wanawake kwenye mnyororo wa umasikini kiasi cha wao kujiingiza katika biashara ya ngono ili kujikwamua kiuchumi. Katika mazingira haya, ni vigumu sana kwa wanawake kutimiza ndoto yao ya kupata maisha bora na yenye usawa na haki kama inavyojadiliwa na wanaharakati wa kifeministi. Mwandishi anaonesha kuwa kikwazo cha uchumi kinawafanya wanawake hata kuwa na tamaa ya pesa na kuithamini zaidi kuliko hata uhai. Mfano mzuri katika riwaya hii ya *Salamu Kutoka Kuzimu* ni *Waridi*, binti ambaye kutokana na tamaa ya pesa anaamua kumuua mpenzi wake ili achukue fedha zake zote. Wakiwa katika starehe, *Bomba*, ambaye ni mpenzi wake *Waridi* anamwambia *Waridi* waachane kitu ambacho kinamkasirisha zaidi *Waridi* kwa kuona

kwamba atakosa mtu ambaye anaweza kuwa anampa pesa kama *Bomba* anavyofanya. Mwandishi anasema:

"*Kijana huyu mwenye asili ya Kiarabu alikuwa mtu ambaye Maua alimhitaji. Siku zote alionekana amejaa. Fedha kwake hazikuwa na tatizo.Wala hakuona uchungu kutumia fedha hizo. Kadhalika fedha zake hazikukaa mfukoni kama wanaume wengine. Kitita cha elfu kumi au ishirini kikiwa kimefungwa kwa mpira kingekaaje mfukoni? Kwa hivyo Waridi alizoea kutimiza mahitaji yake kwa kutumia fedha hizo. Waridi anaona atakuwa na shida sana kuanza tena kujitafutia riziki". (uk.10).* Hii inadhihirisha kuwa mazingira magumu ya kiuchumi aliyolelewa Waridi yamemfanya awe na tamaa ya fedha zaidi badala ya kuthamini mapenzi anayopewa. Tabia hii ambayo amekua nayo tangu utotoni inamfanya asiwe muoga hata kuiba ilimradi aweze kupata fedha. Mwandishi anamuelezea Waridi akirudi chumbani baada ya kuona Bomba akiwa anaoga bafuni, lengo kuu ni kuiba pesa ambazo Bomba ameziacha kwenye mfuko. Alipouendea mfuko na kuufunua alikuta furushi kubwa la pesa ambazo hajawahi kuziona katika maisha yake. Mwandishi anatueleza kuwa "*Waridi akajishauri kuchota kidogo azifiche. Kisha akasita. Alizihitaji zote, akaamua kuzipata*" (uk.11). Hii inaonesha kuwa wanawake wamechorwa kama watu wasio waaminifu katika mapenzi na kwamba wapo tayari hata kuua ili wapate pesa. Tabia hizi ni miongoni mwa tabia zinazokinzana na dira na muelekeo wa wanaharakati wa ufeministi lakini pia chanzo cha tabia hii wanayokuwanayo wanawake ndiyo chanzo kikubwa kinachokwamisha ndoto za wafeministi.

**VIKWAZO VYA KIMAZINGIRA**

Tumekwisha ona mazingira yanayowaweka wanawake katika vikwazo vya kiuchumi. Kwa upande mwingine, mazingira yanayowazunguka watu pamoja na maisha au matukio wanayopitia katika maisha yao huwafanya kupoteza muelekeo wa maisha na kuwafanya kuwa na roho mbaya pamoja na chuki dhidi ya binadamu wenzao. Mfano, riwaya ya *Mtambo wa Mauti* (2004) tunaona muhusika mkuu aitwaye Mona Lisa au Margareth akigeuka na kuwa muuaji hatari sana wa watu. Mwandishi anaonesha dhahiri kuwa tabia ya Mona Lisa imetokana na mazingira yaliyomfanya kuwa na roho ya kikatili na kujiingiza kwenye shughuli za kihalifu. Kitendo cha mama yake mzazi kuuawa kikatili angali Mona Lisa akiwa mdogo kinachochea tabia ya muhusika huyu kuchukia wanadamu na kuona kitendo cha kuua kama cha kawaida. Tofauti na mama yake mzazi, dada yake kipenzi pia anauawa kinyama kitu kinachomfanya kutaka kulipa kisasi. Hata hivyo, mazingira ya ukatili kwa Mona Lisa hayajaishia hapo kwani baba yake mlezi anaamua kumbaka Mona Lisa kwa tamaa ya mapenzi kitu ambacho kinachochea zaidi roho ya kikatili kwa binti huyu. Vilevile, Morlene Johnson, muhusika ambaye anaoneshwa kuishi na Mona Lisa ni mtu anaefanya shughuli za mauaji na uangamizaji wa watu. Mazingira yote haya anayokulia Mona Lisa ni darasa huru linalojitosheleza kabisa kumfanya aige tabia ya watu wanaomzunguka kwani mazingira anayoishi mtu humfunza tabia mbalimbali kama vile Cohen (2012) anavyounga mkono hoja kwa kudai kwamba sababu za kijamii na mazingira ndiyo chanzo kikubwa ambacho humfanya mtu awe na tabia mbaya au nzuri. Hivyo basi, tunaona kwamba mazingira yanayowazunguka wanawake bado ni changamoto kubwa katika kuwakomboa kifikra, kiuchumi na kijamii. Taswira hasi za wahusika kama ilivyo katika riwaya hizi hazishabihiani na malengo ya wafeministi ambao wanapigania uhuru wa mwanamke kutoka kwenye mfumo dume ambao umekuwa ukiwakandamiza kwa muda mrefu.

**VIKWAZO VYA KIJINSIA**

Vikwazo vya kijinsia ni miongoni mwa changamoto ambazo unaweza kuzipata ndani ya riwaya za Ben Mtobwa.

Mfumo dume unaposhamiri, ni wanawake ambao huumia zaidi kutokana na tofauti za kijinsia zilizopo kati yao na wanaume. Katika riwaya za Ben Mtobwa, wanawake wanachorwa kama viumbe dhaifu sana mikononi mwa wanaume na kwamba wanatumiwa kama chombo cha starehe lakini pia wanatumika katika kufanikisha harakati za mauaji yanayotekelezwa na wahusika wa kiume. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* tunaona namna wahusika wa kike wanavyotumika kama chambo katika kutekeleza uhalifu na mauaji. *Proper*, ambaye ni muhusika maarufu kwa kufanya mauaji kwenye riwaya hii, anamtumia *Waridi* kumsogeza Joram katika anga zake za mauaji. Waridi ananunuliwa nguo zinazoacha maungo yake wazi ili amvutie zaidi Joramu na aweze kutekeleza mpango wa kumpa sumu kama alivyoagizwa na Proper. Katika riwaya hii, Proper anamuambia Waridi:

"*Ondoa hiyo mikunjo ya hofu uvae sura yako nzuri kama ilivyo. Akija mpe tabasamu, mpe mapenzi, "kisha mkaribishe pombe. Usisahau chupa hiyo hapo ni yake, asipoinywa mpake hii kwa hila*" (uk.22). Kinyume na hiari yake, tunaona kwamba Waridi analazimishwa kufanya matendo hayo ya kikatili kutokana na udhaifu wake wa kijinsia na anapokataa anabakwa pamoja na kupokea vitisho mbalimbali ikiwemo kutishiwa kushtakiwa juu ya mauaji ambayo alishayafanya huko nyuma. Proper anasema;

"Huendi hata nikisema kuwa Bomba ni ndugu yangu na ninafahamu alikozikwa?'' (uk.5). Maneno haya yanammaliza nguvu na kumfanya atii amri kutoka kwa Proper kitu ambacho kinasababishwa tu na kukosa nguvu kwakuwa yeye ni mwanamke.

Muhusika mwingine anaeathirika na ukatili kutokana na udhaifu wa jinsia yake ni Neema. Katika riwaya hii tunaelezwa kwamba Neema analazimika kujifanya malaya ili aweze kupeleleza mauaji ya watu mbalimbali. Mfano katika ukurasa wa 46 wa riwaya hii, tunaambiwa kwamba "*Ilibidi Neema ajifanye malaya ili aingie katika jumba la mkubwa huyo*" na ndipo alipoweza kugundua siri za mauaji ya watu mbalimbali. Kitendo cha kutumika katika shughuli za upelelezi kinawaingiza wanawake katika mazingira hatarishi kwani hata wahalifu wanatumia udhaifu wao kuwabaka, kuwanyanyasa na hata kuwaua. Kwa mtazamo wa kifeministi, ni dhahiri kwamba itakuwa kazi ngumu sana kuupata usawa ikiwa wanawake wanaendelea kuchorwa kama viumbe dhaifu ambao wanaweza kutumiwa na wanaume katika mipango yoyote ile pasipo hiari yao.

**TASWIRA ZA WANAWAKE KATIKA RIWAYA ZA BEN MTOBWA**

Ni dhahiri kuwa taswira za wahusika wa kike katika riwaya za Ben Mtobwa ni hasi kwa kiasi kikubwa. Wanawake katika riwaya hizi wamechorwa katika sura ambazo hazipendezi machoni mwa jamii na kwamba hawawezi kuwa mfano wa kuigwa. Makala haya yamegundua taswira zifuatazo kwa wahusika wa kike katika riwaya teule za Ben Mtobwa.

**Wanawake kama Makahaba**

Wanawake katika riwaya hizi wamechorwa kama watu wanaojihusisha na ukahaba ili kujipatia fedha kwaajili ya kujikwamua kiuchumi. Biashara ya ukahaba inaonekana kufanywa na wakubwa na kurithishwa kwa watoto kupitia malezi kama tunavyoona katika *Dar es Salaam Usiku* jinsi Rukia alivyoanza kujifunza kufanya ukahaba. Mwandishi anasema ;

'*Wateja wa mama yake walipokuja kumtafuta na kumkuta yeye walimtazama kwa tamaa, lakini walisita. Ututo wake na macho yake meupe yasiyo na hatia, yaliwatisha. Wakaondoka zao huku wakimeza mate. Kitu kimoja watu hawa hawakufahamu. Hawakuwa na habari kuwa mtoto huyu alikuwa tayari kwa lolote na chochote. Tayari kufanya safari yoyote ya kheri au shari hata iwe kwenda mwisho wa dunia. Hala hakuwa mgeni kwa lolote kama walivyodhani wao. Tangu alipopata uhai na kuanza kupambanua mambo, alikuwa ameshuhudia mama yake akitupwa chali au kifudifudi kutendewa kila kitu, mara kwa mara*" (Uk 3)

**Chombo cha starehe**

Wanawake wamechorwa kama chombo cha starehe kwaajili ya wanaume. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* mwandishi amemtumia Proper kama mwanaume anayefurahia kutumia wanawake kimapenzi kabla ya kuwaua. Mfano mzuri ni pale Nuru anaokolewa na Joram aliyekuwa anaishi katika hoteli hiyo kwa kutumia jina Duncan. Tunaambiwa Proper alikuwa akimwambia Nuru, "*Umekuwa msichana mzuri sana. Hufai kufa bila kuonjwa*." Hapo ndipo Joram alitokea na kuokoa maisha ya Nuru (uk.118). Inabainika wazi hapa kwamba wanawake wanatumika kama chombo cha starehe kwa wanaume bila hiari yao. Taswira kama hii haipendezi machoni mwa wafeministi kwani inamdhalilisha mwanamke katika jamii inayomzunguka.

**Chambo katika Upelelezi**

Wanawake wanachorwa kama chambo wanaotumiwa na wahalifu katika upelelezi. Kitendo cha wanawake hawa kukubali kutumiwa na wahalifu katika shughuli za upelelezi kinadhihirisha kwamba wanawake wanajihusisha na kazi ambazo haziwafai kwani wanajiingiza katika mazingira hatarishi. Mfano, kwenye Salamu

Kutoka Kuzimu Neema anatumiwa na Proper katika kutekeleza shughuli za upelelezi na majaribio ya kuua watu. Shughuli hizi zinamuweka hatarini pale anaposhindwa kutekeleza majukumu aliyopewa na Proper. Proper anampa Neema dawa za kulevya na kumnajisi kabla ya kumuua. Neema anapozinduka kutoka kwenye usingizi mzito, anajikuta akiwa uchi wa mnyama. Mwandishi anasema, "*Alijikuta kalala uchi kando ya Proper ambaye alikuwa kamkamata kwa mkono mmoja wa pili ukichezea chuchu zake*" (uk.55). Neema anasikitika sana na unyonge wake wa kuwa mwanamke, anakosa nguvu za kujinasua kutoka kwenye mikono wa Proper. Anajaribu kujinasua lakini Proper, kwa kuwa ni mwanaume, anamzidi Neema Nguvu na kumfanya ashangae kile kinachoendelea. Neema anapofoka na kumuuliza kinachotokea, Proper anamcheka tu na kumwambia wanafanya mapenzi.

Hivyo taswira hizi zinatokana na mazingira ambayo wanajihusisha wahusika hawa.

**Hitimisho**

Taswira hasi za wahusika wa kike katika riwaya za Ben Mtobwa hazijachorwa kwa lengo la kuwadidimiza wanawake. Ben Mtobwa anaonesha jinsi dunia ya sasa ilivyotawaliwa na watu waliojaa unafiki, ufidhuli na ukosefu wa utu. Taswira hizi za wanawake katika riwaya hizi zinatoa picha kamili ya changamoto zinazowakabili wanawake katika maisha halisi ya jamii zetu. Hivyo basi, makala haya hayaoni kama taswira hizi ni pigo kwa wafeministi, bali yanaona kuwa taswira za wanawake katika riwaya hizi zimetokana na mazingira yenye changamoto kedekede yanayowazunguka wanawake. Makala haya yanapendekeza kwamba:

(a) Wanawake kwa kushirikiana na serikali wajitahidi kuweka mikakati itakayowakwamua kiuchumi ili kuondokana na mazingira yanayowafanya wakumbane na changamoto zinazowapa taswira hasi katika jamii. Kuwachora wanawake katika taswira safi na nadhifu kwenye kazi za Sanaa hakutosaidia kuepukana na vikwazo ambavyo vinakwamisha malengo ya wafeministi katika kupigania usawa wa kijinsia.

(b) Wanawake wapewe kipaumbele katika elimu. Elimu ni ngao muhimu sana katika kuutafuta usawa wa jinsia kwani itamfanya mwanamke ajitambue yeye kama binadamu anayestahili kupewa haki zake za msingi. Ukosefu wa elimu unawaweka wanawake katika mazingira magumu na kujikuta wakidhulumiwa haki zao.

**MAREJELEO**


Cohen, B, S (2012) Zero Degrees on Empathy: A New Theory of Human Cruelity.London. Allen Lane

Gromov, D. M (2008) 'Mahojiano na Ben R. Mtobwa' katika Kiswahili Forum 15: Kongamano la Tisa la Janheinz Jahn: Mainz.Group Limited.

Kimani, C. (2003). Swala la Dhuluma dhidi ya wanawake katika Fasihi Andishi ya Kiswahili.Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, (Haijachapishwa).

Mtobwa R, B (1984). Salamu Kutoka Kuzimu. Dar es Salaam: Mkuki Publishers.

Mtobwa R, B (1997). Zawadi Ya Ushindi. Dar es Salaam: Heko Publishers

Mtobwa R, B (1998). Dar es Salaam Usiku. Dar es Salaam: East African Publishers

Mtobwa, R B (2004). Mtambo wa Mauti.Nairobi: Vide –Muwa Publishers.

Mtobwa, R. B (1987). Tutarudi na Roho Zetu. Dar es Salaam: Mkuki publisher.

Ndungo, C.M. (1998). Images of Women in Gikuyu Oral literature: A Case of Gikuyu and Swahili Proverbs. Unpublished PhD Thesis. Kenyatta University.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ogundipe-Leslie, O. (1994). African Women and Critical Transformations. Trenton: African World Press.

Pamela, A.A. (2016). Usawiri wa Uovu katika Riwaya Teule za Ben R. Mtobwa. *Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.*

Ruthven, K.K. (1990). Feminist Literary Studies: An Introduction. Cambridge: Cambridge University Press

Steady, F.C. (1981): Black Women Cross- Culturally. Cambridge: Scherkman Publishing Co

Wamitila K.W. (2003) Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia. Nairobi Focus Publications.